ISO 9001:2015 Certified

# The Regulator

JARIDA LA KILA ROBO MWAKA LA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

Linatolewa bure

ISSN: 0856 - 8030 NA. 4/2024 OKTOBA - DESEMBA 2024

## TCRA juu kimataifa viwango sanifu vipya usimamizi

### Utambulisho wa Tanzania Mtandaoni



# Tafiti zinazotekelezwa mwaka wa fedha 2024/2025

Ili kusimamia kwa ufanisi sekta ya mawasiliano inayoendelea kubadilika, TCRA inahitaji kuwa na taarifa muhimu na uwezo wa kujipanga kukabiliana kwa usahihi na masuala mapya na mabadiliko yanayojitokeza katika sekta. Hali hii inahitaji kufanyika, kwenye maeneo ya kimkakati, utafiti ambao matokeo yake yatatumika kwenye shughuli za TCRA. Kwa muktadha huu, baada ya mchakato wa zabuni iliyotangazwa na kushindanisha watafiti wengi, TCRA imewapa watafiti kadhaa kazi za kufanya utafiti kwenye maeneo mbalimbali. Tafiti zinazoendelea ziko kwenye maeneo yaliyoainishwa hapa chini:

**Tafiti zinazoendelea ziko kwenye maeneo yaliyoainishwa hapa chini:**

| Na. | Mada za Utafiti | Malengo ya Utafiti | Muda | Tarehe ya kuanza | Tarehe ya kukamilisha | Taasisi inayofanya utafiti | Kiongozi wa timu ya watafiti | Nchi iliko taasisi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kupitia mfumo wa Kisheria na Kiusimamizi wa sekta ndogo ya utangazaji | Kupitia mfumo wa Kisheria na Kiusimamizi wa huduma za utangazaji kwa kuzingatia maendeleo ya teknolojia za utangazaji na changamoto za sekta ndogo ya utangazaji | Miezi 8 | Mei 2025 | Februari 2025 | M/S Cenerva Ltd | Prof. H.Sama Nwana | Uingereza |
| 2 | Durusi kuhusu kuridhika kwa Watumiaji wa huduma na bidhaa | Kubaini kiwango cha ubora wa huduma za mawasiliano na namna watumiaji wa wanavyoridhika na huduma hizo. | Miezi 5 | Januari 2025 | Juni 2025 | Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) | Dkt. Deogratius Lashayo | Tanzania |
| 3 | Durusi kuhusu kuridhika kwa Wateja wa TCRA | Kupima viwango vya namna wateja wa TCRA wanavyoridhika na huduma zinazotolewa kwa kuzingatia utendaji unavyofanyika kama inavyoelekezwa kwenye vipimo vya ufanisi vya ISO 9001:2015 na Mkataba wa TCRA wa Huduma kwa Wateja | Miezi 5 | Januari 2025 | Juni 2025 | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) | Prof. Siasa Mzenzi | Tanzania |
| 4 | Teknolojia zinazojitokeza | Kuweka mfumo wa usimamizi wa Akili Mnemba Tanzania | Miezi 6 | Januari 2025 | Juni 2025 | Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es Salaam (DARTU) | Dkt. Godfrey Wandwi | Tanzania |

ISSN: 0856 - 8030
NAMBA YA USAJILI: 00000115
Na. 4/2024. OKTOBA - DESEMBA, 2024

# The Regulator

Hili ni toleo la Kiswahili la jarida la The Regulator, linalotolewa mara nne kwa mwaka na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). TCRA ni taasisi ya serikali inayosimamia mawasiliano ya kielektroniki na posta nchini. Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

## Sheria Na. 12 ya mwaka 2003 iliyoianzisha TCRA inaipa Mamlaka wajibu katika majukumu yafuatayo:

1. Kukuza ushindani bora na uchumi wenye tija;
2. Kulinda maslahi ya watumiaji;
3. Kulinda mitaji ya Watoa Huduma wenye ufanisi;
4. Kukuza upatikanaji wa huduma zinazodhibitiwa kwa watumiaji wote wakiwamo wenye kipato kidogo, walioko vijijini na watumiaji walio na walioko katika mazingira magumu;
5. Kuimarisha Elimu kwa Umma, uelewa na ufahamu wa huduma zinazosimamiwa na TCRA, ikiwa ni pamoja na:
   (i) Haki na wajibu wa watumiaji na watoa huduma zinazosimamiwa;
   (ii) Namna ya kuwasilisha malalamiko na migogoro na utaratibu wa utatuzi wake; na
   (iii) Kazi na majukumu ya Mamlaka kwa kuzingatia umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira.

## MKAKATI WA TCRA 2021/22-2025/26 NA MALENGO YA KIMKAKATI

Mamlaka imeandaa Malengo mbalimbali ili kufikia maono yake katika kukabiliana na mambo muhimu kama yalivyobainishwa katika uchambuzi wa hali halisi ya kisekta. Malengo hayo ni:-

1. Kukuza miundombinu na huduma za mawasiliano ya kielektroni na posta yenye usalama, ufanisi na imara;
2. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya kielektroni na posta zenye ubora na unafuu;
3. Kuimarisha ubunifu wa huduma zinazodhibitiwa, uandaaji wa maudhui ya ndani na ujanibishaji;
4. Kuimarisha ufanisi wa huduma zinazodhibitiwa na kuwalinda wadau; na
5. Kuimarisha uwezo wa taasisi.

## MATOKEO YA MKAKATI

1. Kupatikana kwa huduma za mawasiliano za uhakika na salama;
2. Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano zilizo bora na nafuu;
3. Jamii yenye kuzalisha na kutumia maudhui ya ndani;
4. Kukua kwa ufanisi wa sekta ya mawasiliano na uzingatiaji wa sheria, kanuni, miongozo, kanuni ndogo na viwango kwa wadau wa sekta ya mawasiliano; na
5. Kuongezeka kwa ufanisi wa kiutendaji wa taasisi.

## SERA YA UBORA

Kutokana na nguvu za kisheria za kusimamia sekta za Mawasiliano ya Kielektroni na Posta Tanzania, TCRA imejidhatiti kuweka mazingira mazuri kwa Wenye Leseni kwa kutoa rasilimali, kudumisha na kuendelea kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Ubora ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora na nafuu kwa watumiaji ili kukidhi matakwa ya Sheria na ya kiudhibiti.

## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Mhandisi. Mwesigwa Felician

**Katibu**
Bw. Rolf Kibaja

**Wajumbe**
Bw. Semu Mwakyanjala (Mratibu)
Dkt. Philip Filikunjombe
Bw. Peter Lyimo
Bw. Robin Ulikaye
Bw. Abel John
Bi. Vitalia Kidabulo
Bw. Alpha Wawa

**Mhariri Uzalishaji**
Bw. Isaac Mruma

**Anwani ya ofisi za uhariri**
Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 474,
Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu: +255 784558270, +255 784558271.
Barua pepe: regulator.magazine@tcra.go.tz;
dg@tcra.go.tz
@tcra_tanzania

# Yaliyomo


04 Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu



13 Kanuni takaelelektroniki zaboreshwa



Mapya kwenye sheria

05 TCRA juu kimataifa viwango sanifu vipya usimamizi



Makala kuu

15 Huduma intaneti zaimarika, ulaghai mitandaoni wapungua




Ripoti

06 TCRA kugawa masafa kwa mnada Julai




Intaneti

22 Takwimu sekta ya Mawasiliano



BARUA YA MHARIRI

# Zana usimamizi mpya, ripoti ya mwaka

Makala kuu ya toleo hili inaeleza jinsi Shirika la Mawasiliano Ulimwenguni (ITU) unavyoirodhesha Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuwa miongoni mwa vyombo vya uangalizi vyenye zana muhimu za kufikia kiwango cha juu cha usimamizi.

Tuna ripoti mbili zinazothibitisha jinsi TCRA inavyotekeleza udhibiti shirikishi, mojawapo ya viwezeshaji muhimu kwenye mpito kuelekea uchumi wa kidijiti.

Ripoti hizi zinaonyesha kuwa Tanzania ina alama zaidi ya wastani wa Afrika kwenye nguzo zote nne za udhibiti shirikishi na viashiria vyake.

Pia tunatoa taarifa jinsi Tanzania inavyoanzisha kituo kinachowezeshwa na ITU ili kuongeza kasi ya mabadiliko ya kidijitali nchini kupitia uvumbuzi wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

TCRA inakuza uvumbuzi na kusaidia wajasiriamali wanaotumia vipaji na ujuzi wao kubuni miradi inayochangia maendeleo ya teknolojia na huduma za mawasiliano na pia inayolenga kuchangia ajenda ya uchumi wa kidijitali wa Tanzania.

Mkurugenzi Mkuu Dkt. Jabiri Bakari ni mjumbe ya bodi ya ITU ya Ubunifu na Uvumbuzi wa Kidijiti.



Tumeanzisha jukwaa la kujadili mada mbalimbali kuhusu teknolojia na huduma za mawasiliano. Makala ya uzinduzi inazungumzia chaguo za matumizi ya setilaiti na waya za faiba kutoa kutoa huduma za intaneti ya kasi.

Tuna vidokezo muhimu kutoka kwenye Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura uliotolewa na TCRA hivi karibuni, Mpango huo unaainisha mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuwasiliana kwenye hali ya maafa na uokoaji, kama ilivyotokea Novemba mwaka huu baada ya kuanguka jengo la biashara eneo la Kariakoo, Dar es Salaam.

Toleo hili la mwisho wa mwaka linawasilisha na kuchambua takwimu za mawasiliano za Oktoba - Desemba na za mwaka 2024.





Jarida hili linakuwezesha kupitia na kupata stadi mpya na pia kupanua mtandao wako wa watu wenye weledi kama wewe. Kupata nakala za bure za jarida hili na kuwasilisha maoni, tuma barua pepe kwa

regulator.magazine@tcra.go.tz | barua@tcra.go.tz

Soma kujisajili

Tunakaribisha maoni na hoja kutoka kwa wasomaji wetu. Kwa maelezo zaidi tafadhali piga simu ya bure kwenye namba ya wateja wa TCRA, ambayo ni **0800008272.**

UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU

# Mpango wa mawasiliano kufanikisha usimamizi maafa



Dkt. Jabiri K. Bakari, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeandaa na kuchapisha Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura unaoainisha mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuwasiliana katika kipindi cha maafa.

Mpango huo wa kimkakati unakusudia kutambua uwezo unaohitajika kwa watoa huduma za dharura na namna ya kuwasiliana katika hatua zote za usimamizi wa maafa.

Lengo ni kuhakikisha kuwepo utangamani wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano wakati wa matukio yasiyotarajiwa yanaylosababisha uharibifu, maangamizi na mateso makubwa ya kibinadamu ambayo yako nje ya uwezo wake. Kwa hali hii waathirika wanahitaji msaada wa nje ngazi ya kitaifa au kimataifa.

Mpango huo unakusudiwa kutambua uwezo wa watoa huduma za dharura kimawasiliano na pia vikwazo katika usambazaji mifumo ya mawasiliano, alifafanua.

Vilevile unatarajiwa kufanikisha mawasiliano wakati wa maafa kama yale mafuriko ya Rufiji na Hanang na kuporomoka kwa jengo la biashara Dar es Salaam ambako watu kadhaa walipoteza maisha.

Dkt Bakari amesema Mpango huo unaelezea namna ya kudhibiti vihatarishi kwa kuimarisha mawasiliano kwenye hatua zote za shughuli za kiserikali, za umma, sekta binafsi na za jamii iliyoko kwenye vihatarishi husika

Vilevile unasisitiza umuhimu wa kuchambua vihatarishi muhimu vya miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Miundombinu hii inaweza kuathiriwa na maafa ya asili, mafuriko, kukumbwa na vimbunga au shughuli za kibinadamu na hujuma.

Vihatarishi ni jambo au kitu chochote kinachoweza kwenda mrama na kuleta athari hasi zinazoweza kusababisha maafa. Mpango wowote wa kuthibiti vihatarishi unatakiwa kuweka utaratibu wa kuvipunguza, kufanya maandalizi ya kukabiliana navyo vinapotokea na kurejesha hali ya awali.

TCRA itazingatia mahitaji na kuharakisha utoaji wa leseni zitakazofanikisha usimamizi wa maafa  na masuala ya dharura. Leseni hizo ni pamoja na masafa, namba na idhini ya vifaa vya mawasiliano vinavyoruhusiwa kutumika Tanzania.

Lengo ni kuhakikisha kwamba huduma zinazowezeshwa na miundombinu ya mawasiliano iliyoathirwa na maafa zinarejeshwa ndani ya saa 24.

Mpango huo unawataka wadau kufanya mafunzo ya mara kwa mara ya namna ya kushughulikia vikwazo vya mawasiliano wakati wa majanga na maafa.

Vilevile wanatakiwa kuwa na utaratibu wa kutambua, kuchambua na kuchukua hatua kuimarisha njia za mawasiliano ili ziendelee kutumika wakati wa maafa.

TCRA itapitia mpango huo kila baada ya miaka mitatu na kuuboresha. Hatua hii itazingatia maendeleo ya teknolojia za mawasiliano na uzoefu kwenye kusimamia maafa.

MAKALA KUU

# TCRA juu kimataifa viwango sanifu vipya usimamizi

Shirika la Mawasiliano Ulimwenguni (ITU) limesema Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inaelekea vizuri kwenye aina mpya ya usimamizi wenye kiwango sanifu cha kimataifa.

ITU inathibitisha katika ripoti ya hivi karibuni kwamba TCRA ina nyenzo zote muhimu kuelekea daraja la juu zaidi la usimamizi unaozingatia miongozo na kanuni imara kuliko utaratibu wa kawaida.

Ripoti hiyo ni sehemu ya mfululizo wa durusi za mifano kuhusu usimamizi unaoshirikisha wadau wengi.

Durusi hizi zinawasilisha upeo wa nchi husika kwenye usimamizi, masuala yanayowezesha ufanisi na zinaainisha maeneo ya kuzingatia ili kwenda mbele.

Durusi hizi zinaweka viwango ambavyo ITU inaviita vya uzao wa tano wa usimamizi.

Uzao huo, unaoitwa 5G, unazingatia viwango vinavohimiza na kuwezesha ushirikiano katika usimamizi wa sekta mtambuka, ripoti hiyo inafafanua.

Usimamizi huu pia ni shirikishi kwa wadau wote kwenye shughuli zinazohusiana na mawasiliano.

ITU inaitaja TCRA kuwa ni msimamizi aliyepevuka ambaye anatumia nyenzo zinazomwezesha kuingia kiwango cha usimamizi cha 5G.

Baadhi ya mambo yanayoleta ufanisi ni sera na kanuni za kuchangia miundombinu, mifumo inayowezesha ushiriki wa wengi na usajili wa laini za simu. Hivi vinawezesha ujenzi wa uchumi wa kidijiti.

Vidokezo muhimu kutoka kwenye ripoti hiyo inayoitwa: Tanzania Msingi imara kuelekea usimamizi kiwango cha 5G.

Uwezo wa kushirikiana kwa namna inayoleta tija ni mojawapo ya misingi imara ya uchumi wa kidijiti na pia ishara muhimu ya kuwepo msimamizi wa kiwango cha 5G.

Ushirikiano ni kipengele muhimu cha usimamizi wa kisasa wa masuala ya kidijiti ni alama ya usimamizi wa viwango vya 5G.



Unapima upana na kina cha ushirikiano wa sekta mtambuka kati ya msimamizi wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na taasisi nyingine zenye shughuli kama yake ambazo zina majukumu kwenye uchumi wa kidijiti.

Usimamizi umewezesha kuingia kwa wahusika ambao wameleta aina ya uvumbuzi na maendeleo vinavyohitajika kwenye soko la mawasiliano kupitia vifaa vya mkononi. Hivyo usimamizi unaongezewa nguvu na wahusika wengine wa kiserikali na kutoka sekta binafsi.

Usimamizi mzuri umewezesha kuwepo ubia kati ya wajasiriamali, kampuni za mawasiliano ya mkononi na taasisi za wahisani kuendeleza teknolojia zinazojitosheleza kwenye afya, huduma na kilimo.

Ni muhimu kuweka vivutio kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi kwenye kuweka na kusambaza miundombinu, kuzalisha ajira na kuendeleza ukuzaji wa stadi na mambo mengine.



Kwa muda mrefu Tanzania imetambua kuwa kusimamia mawasiliano kwa kila taasisi kufanya mambo kivyake kunarudisha nyuma juhudi na kunazuia uvumbuzi, ushindani na ukuaji.

Kwa hali hiyo, Tanzania imetambua kwamba kwenye zama wa kidijiti, iwapo nchi inataka kuvuna faida za mawasiliano ya kasi na teknolojia za kidijiti, mfumo wa usimamizi lazima uwezeshe kuingia wadau wengi sokoni, na uvumbuzi.

Vile vile mfumo wa usimamizi lazima utambue kwamba misingi ya usimamizi wa ushirikiano lazima utumike pote kwenye sekta ya TEHAMA na uchumi.

# TCRA kutoa masafa kwa mnada Julai 2025

Na Mwandishi wetu

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania itagawa kwa mnada masafa kwa mawasiliano ya simu na intaneti Julai mwaka huu, hatua ya kiusimamizi itakayochangia kuharakisha ajenda ya uchumi wa kidijitali nchini, imefahamika.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Jabiri Bakari amesema mnada huo utahusisha vitalu vinne vya masafa katika bendi ya 3600-3800 MHz.

Ameeleza kuwa matumizi ya masafa hayo yataendeleza miundombinu ya mawasiliano ya simu na intaneti ya kasi ambayo itachochea maendeleo ya uchumi wa Tanzania. Masafa hayo yaliyotengwa pia yatawezesha ukuaji wa sekta zote, aliongeza.

“Manufaa mengine ni uwezeshaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi kwenye utoaji wa huduma kama vile elimu, afya, kilimo, biashara, huduma za kifedha kupitia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA)”, Dkt Bakari alieleza.

Alitaja manufaa mengine kuwa ni kuimarisha ubora wa huduma za mawasiliano kwa watumiaji na kupanua utoaji wa huduma za mawasiliano ya simu na intaneti kwa Watanzania wengi zaidi.

**Inaendelea Uk 9.**

# Tanzania kinara usimamizi wa ushirikiano

Na Mwandishi wetu

**Tanzania imetambua kuwa katika zama hizi za kidijiti, iwapo nchi inataka kuvuna faida za mawasiliano ya kasi na teknolojia za kidijiti, mfumo wa usimamizi unatakiwa kuwezesha kuingia sokoni kwa watoa huduma wengi, na uvumbuzi.**

Ripoti nyingine ya Shirika la Mawasiliano ya Simu Ulimwenguni (ITU) inaonesha kuwa Tanzania ina alama zaidi ya wastani wa Afrika kwenye nguzo zote nne za udhibiti shirikishi na viashirio vyake.

Ripoti hiyo, inayoitwa Mtazamo wa Kimataifa wa Udhibiti wa Dijiti kwa mwaka 2023—Sera na Udhibiti ili kuchochea mabadiliko ya kidijitali, inataja nguzo za udhibiti huo.

Ni pamoja na utawala shirikishi wa kitaifa, kanuni za kubuni sera katika nyanja ya kidijitali, zana za ukuzaji kidijitali na ajenda ya nchi kuhusu sera ya uchumi wa kidijitali.

Utawala shirikishi wa kitaifa hupima kikamilifu ushirikiano wa sekta mtambuka miongoni mwa mdhibiti wa TEHAMA, wadhibiti rika na watunga sera. Inashughulikia majukumu ya kitaasisi na ushirikiano rasmi na usio rasmi.

Kwa kuwa, kanuni badala ya sheria huongoza udhibiti wa kisekta, kanuni za muundo wa sera katika nyanja ya dijitali huzingatia uundaji wa mifumo na uwiano wake.

Zana za ukuzaji kidijitali zinajumuisha hatua za udhibiti zinazochochea maendeleo ya uchumi endelevu wa kidijitali.

Kingine kilichojumuishwa hapa ni mahitaji mapya ya watumiaji, miundo ya biashara na mienendo ya soko, usalama wa mtandao, ulinzi wa data, mawasiliano ya simu ya dharura, na uchangiaji wa miundombinu miongoni mwa sekta mbalimbali.

Ripoti hiyo inafafanua ajenda ya sera ya uchumi kidijitali kama sera za nchi na mikakati ya kukuza uchumi wa kidijitali, ujasiriamali na uwekezaji.



Alama ya Tanzania kwa mwaka 2023 kwenye misingi ya muundo wa Sera katika eneo la kidijitali ilikuwa karibu mara mbili ya wastani kwa Afrika.

Ni juu ya wastani wa nchi za Afrika na kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Ripoti hiyo pia inaangazia mikakati mitano ya sera na udhibiti inayochochea mabadiliko ya kidijitali.

Mikakati hiyo ni staili mipya za uongozi zinazotumia mbinu za kimapokeo na za majaribio na ushirikiano wa sekta mtambuka miongoni mwa wadhibiti na watunga sera.

Nyingine ni ushirikiano wa kina wa wadau na kukuza ubunifu.

Wadhibiti katika mfumo mzima wa uchumi wa kidijitali wanapaswa kuimarisha ushirikiano.

Wadhibiti hawa ni pamoja na wale wa sekta ya TEHAMA, fedha, viwanda, nishati na usafiri.

“Ushirikiano wenye ufanisi miongoni mwa wadau ni mojawapo ya viwezeshaji muhimu vya uzingatiaji wa udhibiti na utekelezaji wa sera katika mabadiliko ya kidijitali”, ripoti inasema.

Ushirikiano amilifu na endelevu wa wadau huongeza ubora na umuhimu wa mifumo ya kisheria huku ikiongeza kasi ya uvumbuzi na ujasiriamali katika masoko ya kidijitali, inaongeza ripoti hiyo.

Nchi zinapaswa pia kutekeleza sera na mikakati ili kukuza uchumi wa kidijitali, ujasiriamali na uwekezaji.




*Rais, Dr Samia Suluhu Hassan akizindua mkongo wa faiba unaopita baharini wa 2Africa uliofika Dar es Salaam August 2023*

**Kielelezo 1: Nafasi ya Tanzania katika udhibiti wa sekta mtambuka katika kanda za Afrika, Jumuiya ya Afrika Masharikі (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC)**

| Kiashirio/eneo | Utawala wa kitaifa wa udhibiti na usimamizi | | Misingi ya kuunda sera katika nyanja ya kidijitali | | Zana za Ukuzaji za kidijiti | | Ajenda ya uchumi wa kidijiti | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka | 2021 | 2023 | 2021 | 2023 | 2021 | 2023 | 2021 | 2023 |
| Tanzania | 14.81 | 14.81 | 12.96 | 13.89 | 11.42 | 16.67 | 5.56 | 9.88 |
| Wastani wa SADC | 13.65 | 16.14 | 7.90 | 8.30 | 10.08 | 12.30 | 6.31 | 7.57 |
| Wastani wa EAC | 13.22 | 15.21 | 8.83 | 9.52 | 11.86 | 13.93 | 7.89 | 9.30 |
| Wastani wa Afrika | 13.24 | 15.43 | 7.19 | 7.78 | 10.34 | 12.15 | 6.74 | 7.73 |

# Tanzania, Comoro kushirikiana TEHAMA

Na Mwandishi wetu

Makubaliano ya awali yamefikiwa kuendeleza ushirikiano kati ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Wakala wa Maendeleo ya Huduma za Mtandao nchini Comoro (ANADEN).

Ujumbe wa ANADEN ulitembelea TCRA hivi karibuni kwa ziara ya mafunzo na kubadilishana uzoefu.

Masuala waliyojifunza ni pamoja na yanayochagiza ukuaji wa matumizi ya mtandao kwenye shuguli za serikali na binafsi. Mifano ni utoaji huduma za serikali kupitia mitandao, kikoa cha taifa na kituo cha kitaifa cha taarifa.



*Pichani ni wageni kutoka ANADEN (kushoto) na wenyeji wao (kulia), wakiongozwa na Mkurugenzi wa Masuala ya Kisekta Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; Mhandisi Felician Mwesigwa (katikati) ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu.*

# TCRA kutoa masafa kwa mnada Julai 2025

**(Inatoka Uk 6)**

Matumizi ya masafa hayo pia yatakuza, kuimarisha na kuwezesha ubunifu wa huduma mpya za TEHAMA na matumizi yake.

Ili kuhakikisha kuwa watumiaji wananufaika kikamilifu na huduma za simu na intaneti, Dkt Bakari alisisitiza kuwa TCRA itaweka masharti ya usambazali na utoaji wa huduma kwa matumizi ya masafa husika.

Alifafanua kuwa TCRA itawashirikisha wadau kwenye mchakato wa mnada huo na imeweka ratiba itakayofuatwa kati ya Februari na Juni mwaka huu. Hii inalenga kuwawezesha wadau kujipanga kwa mnada huo.

# Utambulisho wa nchi mtandaoni

Na Mwandishi wetu

Tuanze kwa chemsha bongo kuhusu vitu kwenye nchi mbalimbali ambavyo vinaitambulisha. Jengo la Taj Mahal (India), Ukuta mrefu nchi moja ya Asia (China), mlima wa Everest (Nepal), magari ya Toyota (Japan), mlima Kilimanjaro (Tanzania).

Mtandaoni, ambako mawasiliano yanatumia mifumo ya kompyuta inayohakikisha nchi inapata huduma za intaneti, mataifa yanatambuliwa kwa kitu kinachoitwa Domeini ya Kiwango cha Juu ya Fumbo la Nchi. Kifupisho chake kwa kiingereza ni ccTLD.

Domeini inatumika au imetengwa kwa nchi, dola huru au eneo la nchi linalotambulika kwa msimbo wa nchi. Ina herufi mbili, kwa mfano kwa Tanzania ni TZ, lakini kwa herufi ndogo, yaani 'tz'.

Kompyuta zilizounganishwa kwenye intaneti zina anwani za namba mahsusi zinazozi-wezesha kufikisha taarifa za kielektroniki mahali sahihi.

Mfumo wa Majina ya domeini unatafsiri anwani hizo za namba kwenye kompyuta na kuzipa majina ambayo ni rahisi kutumiwa. Kimawasiliano, anwani hizo zinaandikwa kwa kuanza na nukta (.) kabla ya domeini. Hivyo kwa Tanzania ni dot tz (.tz).

Anwani hizi ni rahisi kukumbuka na vinasaidia watu kupata taarifa kwenye intaneti. Zi-natambulisha raslimali za intaneti kama vile tovuti zilizosajiliwa nchini na ngazi nyingine duniani. Kwa jina lingine, zinaitwa vikoa.

Vikoa vinatumika kutambua kurasa mahsusi za tovuti. Kwa mfano, katika anwani ya tovuti ya "https://www.tcra.go.tz," kikoa ni tcra.go.tz.

Vikoa pia vinatumiwa katika anwani za barua pepe ambazo zinawezesha watu kutuma na kupokea ujumbe wa kielektroniki; kwa mfano, barua@tcra.go.tz.



# TCRA yashirikisha wadau taka za kielekroniki

Na Mwandishi wetu

Tanzania imechukua hatua kuzuia uingizwaji nchini vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki vyenye viashiria vya kuwa ni taka ili kuzuia nchi isiwe jalala ya vifaa vya kielektroniki vilivyotumika.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Dkt. Jabiri Bakari amesema hatua za kisheria na kiusimamizi ni pamoja na kutoza ada ya uchakavu wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki vinavyoingizwa nchini.

Vifaa vinavyoelekea Tanzania vinakaguliwa kule vinakotoka na kutozwa ushuru unaoitwa tozo ya mazingira, ambao utachangia gharama za kuvitekeketeza baada ya kumalizika muda wa matumizi.

Taka za Kielektroniki, au takaelektoniki ni bidhaa na/au vifaa vya kielektroniki vilivyopitwa na wakati na visivyofanya kazi.

Vilevile ni vifaa vilivyokufa ambavyo vina vijenzi vinavyojumuisha vitu hatari na vinasaba vya sumu.



Hivi vinaweza kuhatarisha afya ya binadamu na mazingira vinapotolewa au kutupwa kwa namna isiyofaa. Utupaji sahihi wa taka za kielektroniki unazuia vijenzi hatarishi na vyenye sumu vilivyomo kwenye vifaa vya mawasiliano visiathiri afya ya binadamu na mazingira.

Ada ya mazingira ilianzishwa kuwezesha usimamizi wa utupaji taka zitokanazo na vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki.

Inawapa watengenezaji wajibu wa kuhakikisha vifaa vyao vinatupwa kwa usahihi. Vifaa vyote vya mawasiliano vinavyoingia Tanzania vinakaguliwa kwenye nchi vinakotoka.

Dkt Bakari alikutana hivi karibuni na wawakilishi wa Chama cha Wafanyabiashara wa eneo la Kariakoo Dar es Salaam na aliwafafanulia kuhusu tozo hiyo ya mazingira. Aliwajulisha pia kuhusu hatua nyingine za ki-usimamizi kuhusiana na taka elektroniki.

Kanuni za mwaka 2020 za viwango vya vifaa na usimamizi wa takaelektroniki, ambazo zimerekebishwa 2024 zimeainisha majukumu ya wahusika kwenye mlolongo wa kushughulikia vifaa vya mawasiliano vilivyomaliza muda wa matumizi.

Majukumu haya ni kwa watu wote kwenye mnyororo wote wa utengenezaji, uagizaji, usambazaji, uuzaji, matumizi, uchakataji wa taka na urekebishaji.

Watengenezaji na waagizaji wanatakiwa kuhakikisha kwamba wanaelekeza vifaa vilivyotumika kwa wakusanyaji, wachakataji, waundaji upya na sehemu zilizoidhinishwa za kushughulikia takaelektroniki.

Wanatakiwa pia kuipatia TCRA taarifa za kina kuhusu vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki wanavyoagiza au kutengeneza hapa Tanzania, kulipa ada ya awali ya mazingira na kuhakikisha kwamba vifaa hivyo havijafikia mwisho wa muda wa matumizi.

Makubaliano rasmi pia yafikiwe na wakusanyaji, wachakataji au waundaji wenye leseni za kushughulikia vi-faa vya mawasiliano ya kielektroniki vilivyomaliza muda wa matumizi.

Uingizaji wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki Tanzania unahitaji leseni ya TCRA ya Uingizaji. Vifaa hivyo vinakiwa kuhakikiwa na kukadiriwa gharama na kupitishwa kwa matumizi ili kubaini na kuthibitisha kwamba vinakidhi vigezo vya kuweza kuunganishwa na kutumika kwenye mitandao.

Maombi ya leseni za kuagiza vifaa yatawasilishwa mtandaoni kupitia mfumo ulioko https://verigates.tcra-bureauveritas.co.tz.

Tanzania inafuata kanuni na misingi ya kimataifa katika usimamizi wa taka elektroniki.

Usajili na ukaguzi wa vifaa vya mawasiliano kwenye nchi vinakotoka unazingatia masharti ya Mkataba wa Basel kuhusu Usafirishaji wa Taka Hatarishi Nje ya Mipaka ya nchi na Utupaji wa Taka hizo.

Nchi wanachama wa Umoja wa Mawasiliano Afrika Mashariki (EACO) zina mkakati wa taka elektroniki wa kati ya 2022 na 2027.

Lengo kuu ni kujenga na kuendeleza taratibu za usimamizi endelevu wa taka za kielektroniki kwenye nchi wanachama wa EACO.

Mkakati huo, uliopitishwa na mkutano wa wataalamu ambao TCRA iliandaa mwaka 2023, unataka Afrika Mashariki kuondoa kabisa athari hasi za takaelektroniki kwenye nchi wanachama wa EACO ifikapo mwaka 2030.

Mkakati huo unalenga kuendeleza teknolojia za uchumi unaowezesha mzunguko wa bidhaa. Unataka pia kuendeleza miundombinu ya kushughulikia taka elektroniki na usimamizi wake na kuweka utaratibu wa ku-tumia nguvu za ziada za pamoja kwenye kuendesha miundombinu hiyo.

Mkutano wa hivi karibuni wa TCRA na wawakilishi wa wafanyabiashara Kariakoo ni sehemu ya kampeni ya Mamlaka ya kuongeza uelewa wa wadau kuhusu utupaji salama wa taka elektroniki.

Kariakoo ni kitovu cha biashara za vifaa vya watumiaji huduma za mawasiliano Tanzania.



# Kanuni takaelektroniki zaboreshwa

Na Mwandishi wetu

Kanuni za Usimamizi wa taka zitokanazo na vifaa vya Kielektroniki zimerekebishwa, na majukumu ya ziada yamewekwa kwa wazalishaji na waagizaji wa vifaa vya kielektroniki vitakavyotumika Tanzania.

Marekebisho hayo, yaliyochapishwa katika gazeti la Serikali la tarehe 01/11/2024, yameongeza ufafanuzi na miongozo ya mchakato wa uthibitishaji wa aina ya uidhinishaji. Marekebisho mengine yanawasilishwa kwenye jedwali hapa chini:

### Kanuni ya 17 inaelezea wajibu kwa wazalishaji wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki, ambao ni pamoja na:

i. kuhakikisha kuwa vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki vinavyoletwa sokoni vinakaguliwa mapema ili kuthibitisha kama vimeidhinishwa kwa matumizi;

ii. Kuhakikisha kwamba vifaa vinavyoingia sio taka na vinazingatia viwango vya taka hatarishi vilivyowekwa na sheria husika;

iii. Kusajili TCRA maelezo ya kina ya vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki vinavyoingizwa au kuzalishwa nchini Tanzania;

iv. Kutoa taarifa juu ya eneo lenye taka hatarishi lenye vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki na taratibu za kubomoa vifaa hivyo baada ya kufikia mwisho wake wa matumizi;

v. Kulipa kodi ya awali ya mazingira iliyotajwa katika kanuni hizi kwa ajili ya kushughulikia vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki baada ya mwisho wake wa matumizi wa vifaa hivyo.


**Wazalishaji wanaweza-**

a Kuanzisha mipango na njia za urejeshaji taka za kielektroniki kwa ajili ya usimamizi na uratibishaji wa taka kwa mujibu wa kanuni ya uwajibikaji wa mzalishaji ulioelezewa kwa kina.

b Kuingia makubaliano rasmi na wakusanyaji walioidhinishwa, wachakataji na/au watupaji wa taka au vituo vya uchakataji taka vilivyomo ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano.

Wajibu wa waagizaji bidhaa umeorodheshwa katika kanuni mpya ya 17A ambayo sehemu yake ya 3 inasomeka kuwa:

Muagizaji hapaswi kuagiza vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki vilivyotumika kama vifaa hivyo vimekusudiwa kutupwa au kuchakatwa tena; vinaonyesha kasoro zinazoathiri utendakazi wake; vimechakaa au kuharibika, hivyo kuathiri soko la vifaa hivyo; ambavyo vimekusudiwa kutenganishwa kwa vipuri; au ambavyo vimefikia mwisho wake wa matumizi.



Marekebisho ya Kanuni ya 18 yameongeza majukumu mapya kwa wachakataji na wakarabati. Toleo hili lililojumuishwa linaeleza kuwa wachakataji na wakarabati waliopewa leseni ya kufanya biashara zao nchini Tanzania watakuwa majukumu ya:

i. Kuanzisha michakato ya kuchakata tena au kukarabati vifaa ambavyo ni rafiki kwa mazingira;

ii. Kkuhakikisha uchakataji au ukarabati pamoja na vifaa vyote vinavyotumika katika mchakato huo vinazingatia viwango vya kitaifa na kimataifa;

iii. Kkuhakikisha kwamba mabaki ya taka yanayopatikana wakati wa kuchakata au kukarabati upya yanapelekwa sehemu husika, yaani katika kituo kilichoidhinishwa cha usimamizi wa taka za kielektroniki

iv. Kkuingia katika makubaliano rasmi na wakusanyaji wenye leseni na wasimamizi wa taka za kielektroniki;

v. Kkuhakikisha kwamba vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki vilivyorekebishwa vinakidhi mahitaji ya uidhinishaji wa aina; na

vi. Kkusimamia na kutunza kumbukumbu za vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki vilivyopokelewa kwa ajili ya kuchakatwa au kufanyiwa ukarabati na kufanya kumbukumbu hizo kupatikana kwenye Mamlaka husika.

Kanuni ya 20 juu ya "Wajibu wa watumiaji wakubwa inasema:

Wajibu wa Mtumiaji mkubwa wa vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki ni:

i. Kutenganisha taka za kielektroniki na aina zingine za taka ili kurahisiha zoezi la ukusanyaji wa taka;

ii. Kuuza au kutoa vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki ambavyo vimefikia mwisho wake wa matumizi kwa wakusanyaji wenye leseni, warekebishaji, wachakataji au kwenye vituo vya ukusanyaji wa taka hizo vilivyoidhinishwa;

iii. Kurejesha vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki ambavyo vimefikia mwisho wake wa matumizi kwa wakusanyaji walioidhinishwa;

iv. Kkufuata taratibu zinazopendekezwa za utupaji wa vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki vinapofikia mwisho wake wa matumizi

v. Kutunga sera ya ndani ili kuwezesha usimamizi na uratibishaji wa taka za kielektroniki;

vi. Kusimamia na kutunza kumbukumbu za vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki ambavyo vimefikia mwisho wake wa matumizi na kurahisisha upatikanaji wa kumbukumbu hizo kwenye mamlaka husika wakati zinapohitajika;

vii. Kusaidia katika uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa watumiaji kuhusu udhibiti na usimamizi wa taka za kielektroniki;

vii. Kuingia katika makubaliano rasmi na wakusanyaji wenye leseni, warekebishaji, wasafishaji au vituo vya kusimamia taka hizo; na

vii. Kusaidia uundaji wa vituo vya kukusanya taka za kielektroniki.

Kanuni ya 21 inaorodhesha wajibu wa TCRA.

Inaeleza kuwa Mamlaka-:

i. Itateua mtoa huduma wa nje kwa ajili ya ukaguzi wa awali na kukusanya ada za usimamizi wa mazingira wa vifaa vya kielektroniki vinavyoingizwa katika Jamhuri ya Muungano kupitia mchakato wa kiushindani;

ii. Itaweka rejista (kumbukumbu) ya taarifa za wazalishaji na waagizaji wa vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki vinavyotumika Tanzania;

ii. Itatunza hifadhidata ya vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki vilivyoidhinishwa kutumika nchini Tanzania;

ii. Itawezesha uundaji wa sera za ndani za udhibiti wa taka za kielektroniki kwa watumiaji wengi;

ii. Itaunda mradi wa matumizi ya ada zilizokusanywa za ushuru wa kiikolojia kuhusu usimamizi wa michakato ya mwisho wa matumizi ya vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki; na

ii. itafanya uhamasishaji na kutoa elimu kwa watumiaji juu ya usimamizi wa taka za kielektroniki.

RIPOTI

# Huduma intaneti zaimarika, ulaghai mitandaoni wapungua


Na Mwandishi wetu

Kuenea kwa matumizi ya simu janja kufikia zaidi ya theluthi ama asimilia 36 miongoni mwa watu nchini na kuongezeka kwa kasi ya uunganishaji intaneti majumbani ni kati ya mafanikio makubwa yaliyoshuhudiwa katika sekta ya mawasiliano kati ya Oktoba na Desemba 2024.

Taarifa ya robo mwaka ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Jabiri Bakari inaonesha kuwa ufanisi wa huduma za pesa kwa simu umepishana kati ya mtoa huduma mmoja na mwingine.

Ripoti hiyo inabainisha zaidi kuwa baadhi ya watoa huduma za utangazaji na posta na usafirishaji vifurushi wanakiuka kanuni za ubora wa huduma huku mamlaka ikichukua hatua za kiusimamizi dhidi yao.

Makala hii inawasilisha yaliyojitokeza kwenye taarifa hiyo ya kitakwimu kwa ufupi ili ikusaidia kufahamu yanayojiri ndani ya sekta ya mawasiliano na kufanya maamuzi katika shughuli zako.



## Ongezeko simu janja kuendeleza intaneti

Teknolojia za mawasiliano ya mkononi zinazowezesha intaneti ya kasi zinazidi kuenea Tanzania, ikiwa ni pamoja na asilimia ya simu janja kwa idadi ya watu kuongezeka kwa pointi 11 ndani ya miaka miwili.

Teknolojia za uzao wa tatu (3G) na wa nne (4G) zimeenea miongoni mwa watu kwa wastani wa asilimia 89.5.

Simu janja, yaani zenye uwezo mkubwa zimeenea kwa asilimia 36 miongoni mwa watu mwishoini mwa Desemba, kutoka asilimia 34 Septemba na 25 mwanzoni mwa mwaka 2022.

Simu hizi ni muhimu kwa kupakia na kupakua data, picha na video na zinachangia kuenea matumizi ya intaneti.

Pamoja na simu janja, vifaa vingine vinavyowezesha matumizi ya intaneti pia yameongezeka. Hivi ni pamoja na modemu, ambazo zimeenea kwa watu kwa asilimia 1.02.

Kulikuwa na laini 87,448,346 Desemba 2024 ambazo baadhi zilitumiwa kupitia simu janja 23,419,299 zilitumika mitandaoni. Simu za kawaida, au simu rununu zilikuwa 56,862,957.

Teknolojia ya 3G imeenea miongoni kwa watu kwa asilimia 91, 4G kwa asilimia 88 na uzao wa tano 5G, wenye kasi kubwa ya mtandao, kwa asilimia 22. Aidha, asilimia ya eneo la Tanzania lililofikiwa na mawasiliano ya 3G ni 74 na 4 G ni 71, huku 5G ikifika asilimia 2.5.

Ikilinganishwa na Desemba 2022, kuenea huku kumeongezeka kutoka asilimia 72 kwa 3G na asilimia 55 kwa 4G. Teknolojia ya 5G iliiingia Tanzania mara ya kwanza mwaka 2022.

Mitambo kwenye minara inavyowezesha uzao wa tano, vimeongezeka kwa asilimia nane (8) na kufikia 900, ikiwa zimeenea zaidi maeneo ya mijini. Mikoa inayoongoza kwa vifaa vya 5G, na idadi kwenye mabano ni Dar es Salaam (616 ), Mjini Magharibi ( 58), Dodoma (44), Mwanza (36) na Arusha (32), Mbeya (16), Songwe (13) na Pwani (12).

Mitambo ya kurushia mawimbi ya simu za mkononi inayowezesha 3G imefikia 12,762 na 4G imeongezeka hadi 12,562.

ikiwa zimeenea zaidi maeneo ya mijini. Mikoa inayoongoza kwa vifaa vya 5G, na idadi kwenye mabano ni Dar es Salaam (616 ), Mjini Magharibi ( 58), Dodoma (44), Mwanza (36) na Arusha (32), Mbeya (16), Songwe (13) na Pwani (12).

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa ingawaje mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa wingi wa mitambo ya kurushia mawimbi ya mawasiliano ya 5G na ni kitovu cha mawasiliano Tanzania, Mjini Magharibi unaongoza Tanzania kwa uwiano wa laini zilizosajiliwa na mitambo.

Laini 16,097,634 zimesajiliwa Dar es Salaam na 510,853 Mjini Magharibi. Uwiano wa laini na mitambo ya 5G kwa Dar es Salaam ni 26,133 na Mjini Magharibi ni 8,807.

## Intaneti majumbani yajumuisha watumiaji

Huduma za intaneti kupitia waya za faiba zilizounganishwa majumbani na maofisini na kasi yake vinazidi kuongezeka Tanzania, hali inayoashiria mwelekeo mpya wa utumiaji wa teknolojia zinazojumuisha watu wengi.

Ingawaje teknolojia za faiba nyumbani (FTTH) na ofisini (FTTO) hazijaenea sana Tanzania, zina kasi karibu mara tatu ya teknolojia za simu za vifaa vya mkononi.

Kasi ya teknolojia zinazowezesha intaneti inapitia kipimo cha megabaiti kwa sekunde (Mbps).

Laini 48,028,227 zilitumika kwa huduma za intaneti Desemba 2024. Laini za FTHH zilikuwa 71,660 na FTTO 11,540. Zilizobakia zilitumia njia ya simu za mkononi. FTTO) zina idadi ndogo ya laini 71,661 na 11,540 mtawalia.

Huduma ya intaneti zinatolewa kupitia laini za simu, waya (faiba) na mawimbi. Idadi ya utumiaji wa intaneti inatokana na laini/waya ambazo zimetumia huduma ya Intaneti angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita, bila kujali teknolojia iliyotumika.

Idadi ya utumiaji wa Intaneti imeongezeka kwa 16% kutoka milioni 41.4 kwa robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024 hadi milioni 48 kwa robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2024.

Kasi ya kupakua data kwa teknolojia ya vifaa vya mkononi ilikuwa Mbps 10.8, wakati kwa teknolojia ya FTTH ilikuwa 31.8 Desemba 2024. Ilikuwa 13.2 na 40,9 mtawalia Septemba mwaka jana.

Hadi Desemba 2024 huduma za FTTH na FTTO zilitolewa na kampuni 48 zilizo na leseni ya TCRA ya programu tumizi za mawasiliano.

Usajili wa intaneti ya waya wa faiba unajumuisha usajili wa mtu binafsi na wa taasisi. Teknolojia ya FTTH inawezesha watu wengi zaidi kwenye eneo ilipofungwa kupata huduma kwa mtandao unaowezesha watu wengi kujiunga na chombo kimoja kichounganishwa.

Vilevile inatoa fursa ya watumiaji kupata huduma nyingi zaidi zikiwemo filamu na burudani nyingine wakiwa majumbani.

Wastani wa matumizi kupitia laini hizo ilikuwa ni gigabaiti (Gb) 4.49 kwa laini, ikiwa ni juu ya Gb 4.35 Septemba, uchambuzi wa ripoti umethibitisha.

Hata hivyo, pamoja na laini zinazotumia intaneti kuongezeka kutoka 46,084,364 Oktoba hadi 48,028,227 Desemba 2024, ripoti hiyo inasema watumiaji wa intaneti wanatumia asillimia 10.9 tu ya uwezo wa kuunganisha huduma ya Intaneti kwenda nje ya Tanzania na kuingia nchini.

Tanzania ina uwezo wa Gigabaiti kwa sekunde (Gbps) 17,200.00 kwa ajili ya uunganishaji wa huduma ya Intaneti ambako 1,868.32 tu ndizo zilitumika Desemba 2024. Kuna 15,331.68 zinazosubiri kuunganishwa.

Wakati huo huo vikoa vilivyosajiliwa kwa jina la Tanzania, yaani vyenye dot tz vimeongezeka hadi 32,267 Desemba 2024 kutoka 31,584 mwishoni mwa Septemba 2024.



## Miamala pesa mtandaoni juu, ufanisi wapishana

Miamala ya pesa kwa njia ya simu Tanzania imeongezeka kwa asilimia 25 kati ya Machi na Desemba mwaka jana huku ufanisi ukipishana kwa kiasi kikubwa baina ya mitandao.

Miamala 883,007,283 ilifanywa na akaunti 52,990,091 za pesa mtandao kwenye kampuni sita Machi 2024 ikilinganishwa na miamala 1,100,700,205 kupitia akaunti 63,207,569 Desemba.

Watoa huduma za pesa kwa simu Tanzania na majina ya biashara kwenye mabano ni Airtel (Airtel money), Azam (Azam pesa), Halotel (Halopesa), TTCL (T-pesa), Vodacom (M-pesa), Yas by Mixx zamani Tigo.

Uchambuzi wa takwimu hizo unaonesha kuwa Azam pesa ilikuwa na uwiano mkubwa zaidi wa idadi ya miamala kwa akaunti huku nusu ya akaunti za T-Pesa ya TTCL zikiwa hazikufanya muamala wowote.

Akaunti za pesa kwa simu zilizosajiliwa Azam zilikuwa 32,418 ambazo zilifanya miamala 1,638,250 –wastani wa miamala 50.53 kwa akaunti. Akaunti za T-pesa zilikuwa 1,508,952 zilizofanya miamala 633,850.

Pamoja na kutoa huduma za pesa kwa simu, kampuni ya Azam pia inaongoza kwa kuwa na ving'amuzi vingi zaidi chini ya mfumo wa utangazaji wa televisheni kupitia teknolojia ya ardhini (DTT) na wa setilaiti (DTH), ambavyo matumizi yake yanalipiwa kupitia mitandao pia.

Takwimu zinaonesha Azam ilikuwa na vinga'muzi 1,340,135 kati ya 2,148,763 vilivyokuwa vikitumika Tanzania Desemba 2024.

**Wastani wa uwiano wa miamala na akaunti za pesa mtandao kwa watoa huduma wengine ni:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Airtel Money | 9.7 | Halo Pesa | 6.9 |
| Airtel Money | 4.97 | Halo Pesa | 5.56 |

Uchambuzi zaidi wa takwimu hizo unaonesha kuongezeka kwa laini za simu za mkononi zinazotumika kwa asilimia 65.4 – kutoka 52,885,243 Machi 2021 hadi 87,448,346 Desemba 2024.

### Akaunti za pesa za simu nazo ziliongezeka takriban mara mbili ndani ya miaka minne

Milioni **32.72** 2021 — **89.1%** — Milioni **61.88** 2024

Takwimu zinaonesha baadhi ya watoa huduma wamepoteza akaunti na wengine wameongeza kwa kiasi kikubwa kati ya Oktoba na Desemba 2024.

## Ulaghai kwa simu wapungua, Kilombero bado sugu

Ingawaje kwa ujumla, matukio ya ulaghai kupitia simu za mkononi yamepungua kati ya Septemba na Desemba mwaka jana, kutoka 16,002 mpaka 12,896, Wilaya ya Kilombero imekuwa sugu kwa vitendo vya kilaghai, ikiwa na asilimia 32 ya matukio ya majaribio ya uhalifu.

Ripoti ya ukaguzi wa usalama mitandaoni kati ya Oktoba na Desemba inaonesha kuwa wilaya nyingine zenye idadi kubwa ya matukio ya ulaghai kwa simu za mkononi ni Sumbawanga Mjini, yenye matukio 3,795 au asilimia 29 ya matukio kitaifa, na Sumbawanga Vijijini yenye matukio 1,083 – asilimia 8.

Kati ya jumla ya matukio ya ulaghai kwa simu 12,896 nchini Oktoba hadi Desemba, Kilombero ilikuwa na 4,101, Sumbawanga Mjini 3,795 na Sumbawanga Vijijini 1,083.

Uchambuzi unaonesha kuwa matukio Kilombero yameongezeka kwa asilimia 214, kutoka 1,306 Septemba 2024.

Ulaghai kwa simu wa mkononi unafanyika kwa matapeli kupiga simu au kutuma ujumbe wa kuwahadaa watumiaji wawatumie taarifa zao binafsi za simu na miamala na kuzitumia kuiba kwenye akaunti za simu za mkononi au benki.

Ukaguzi wa robo mwaka iliyoishia Desemba umetaja mikoa tisa yenye matukio zaidi ya 100 ya ulaghai. Rukwa inaongoza kwa matukio 5,308, ikifuatiwa na Morogoro (4,278), Mbeya (930), Dar es Salaam (765), Katavi (281), Arusha (260), Songwe (150), Mwanza (132) na Tabora (122).

Mikoa yenye matukio chini ya 10 ni Kaskazini Pemba (1), Kusini Pemba (2), Kusini Unguja (5), Kaskazini Unguja (5) na Simiyu (7). Mkoa wa Mjini Magharibi ulipunguza matukio 122 Septemba 2024 hadi 15 Desemba.

Watoa huduma wenye matukio mengi na idadi kwenye mabano ni Airtel (5,187), Vodacom (2,901) na TTCL (2,391). Ingawaje Yas, zamani Tigo ina matukio 1,663, kampuni hiyo imeyapunguza yaliyokuwepo Septemba 2024 kwa asilimia 75 – kutoka 6,581.

Tathmini inaonesha kuwa pamoja na Yas, Vodacom imepunguza matukio kwa asilimia tisa, kutoka 3,175 mpaka 2,902.

Kampuni ambazo matukio yameongezeka kulinganisha na Septemba ni TTCL, kwa asilimia 12 kutoka 2,127 mpaka 2,391, Airtel kwa asilimia 52 kutoka 3,408 kufikia 5,187.

TCRA imeendelea kuwachukulia watoa huduma ambao mitandao yao inatumiwa kwa ulaghai ikiwa ni pamoja na hatua za kiudhibiti na kikanuni. Vilevile inatoa elimu kwa watumiaji na umma kwa ujumla kuhusu namna ya kujiloinida mitandaoni na kuripoti uhalifu kwa kutuma taarifa kupitia namba 15040 bia malipo.

Hivi karibuni mawaziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mambo ya Ndani walikutana na wadau wa usalama wa mitandao ya simu na kuainisha hatua za kuthibniti ulaghai mitandaoni ili kujenga imani ya watumiaji, kuimarisha usalama mitandaoni na kupanua ushiriki wa wananchi katika mawasiliamo na masuala ya kifedha.



## TCRA yaonya redio, televisheni zinazokiuka kanuni

TCRA imeonya watoa huduma za utangazaji wanaokiuka vipengele kadhaa vya kanuni za utoaji maudhui kuwa itaendelea kuwachukulia hatua stahiki za kiudhibiti na kiusimamizi.

Hii inafuatia ukaguzi wa kila robo mwaka wa uzingatiaji kanuni za utangazaji na masharti ya leseni kugunduia ukiukwaji kwenye uzingatiaji wa ratiba ya vipindi na dakika zinazotakiwa kwa taarifa ya habari.


Ukaguzi uhusisha maudhui ya televisheni 16 na redio 12 zenye leseni za kitaifa.

Utaratibu wa TCRA wa maombi ya leseni za maudhui ya redio na televisheni unawataka waombaji kueleza jinsi watakavyohakikisha ubora wa vipindi, faida za vipindi kwa uchumi wa jamii. Aidha wanatakiwa kuwasilisha ratiba ya vipindi kabla ya kuanza kuvitoa na kuizingatia. Ratiba inatakiwa kueleza muda, mpangilio, na idadi ya vipindi.

Televisheni sita tu kati ya 16 zilizotathminiwa zilizingatia ratiba iliyowasilishwa TCRA mapema. Hii ni pamoja na kuwa 12 kati ya hizo ziliwasilisha ratiba.

Watoa huduma wamefanya vizuri kwenye utoaji wa maudhui ya ndani, ambapo kanuni zinataka yawe angalau asilimia 60 na kwenye vipindi vya elimu.

Hata hivyo matokeo ya ufuatiliaji huu yanaonesha mabadiliko kulinganisha na Septemba 2024 ambako redio zote 12 zilizopitiwa zillkiuka masharti ya kuzingatia ratiba.



## Wasafirisha vifurushi wakiukaji kanuni washughulikiwa

TCRA imechukua hatua za kiusimamizi dhidi ya watoa huduma za usafirishaji vifurushi ndani ya Tanzania wanaokiuka masharti ya kufikisha vitu vya wateja ndani ya siku moja kama ilivyoainishwa kwenye kKanuni za ubora wa huduma.

TCRA inafanya ukaguzi wa kila robo mwaka kuhusu uzingatiaji wa kanuni za ubora wa huduma umeonesha kuwa nusu ya watoa huduma waliohusishwa hawakukidhi vigezo vya kanuni na masharti ya leseni.

Ukaguzi ulifanywa kwa watoa huduma za usafirishaji vifurushi wa Kanda A, yaani kati ya miji ya Arusha, Moshi, Tanga, Morogoro, Kibaha, Dodoma,Mbeya, Mwanza, Iringa, na Zanzibar.

Vipimo vilizingatia kasi ya huduma toka bidhaa inapokabidhiwa kwenye ofisi ya mtoa huduma hadi inapofikishwa iendako. Wanatakiwa wahakikishe kuwa angalau asilimia 85 ya vitu walivyopokea vinafika kunakotakiwa siku inayofuata.

Kanuni hizo pia zina miji ya kanda B ambamo wasafirishaji wanatakiwa kuhakikisha wanafikisha angalau asilimia 88 ya vitu wanavyopokea ndani ya siku tatu.

Miji hiyo ni Tabora, Shinyanga, Kahama, Bariadi, Geita, Singida, Bukoba, Musoma, Kigoma, Mtwara, Lindi, Songea, Sumbawanga, Songwe, Mpanda, Babati, Njombe, na Mkoani na Chakechake Pemba.

Watoa huduma kwenye kundi hili walikuwa na ufanisi zaidi. Kati ya 13 waliokaguliwa ni wanne tu wasiokidhi matakwa ya kanuni.

Matokeo ya ukaguzi robo mwaka iliyoishia Septemba 2024 yalionesha kuwa watoa huduma 12 kati ya 19 wa kanda A hawakukidhi matakwa ya kanuni.

Hadi Desemba 2024, TCRA ilikuwa imetoa leseni 153 za huduma za posta na usafirishaji wa vifurushi. Kati ya hizo, moja ni ya Posta ya umma – Shirika la Posta Tanzania (TPC). Nyingine na idadi kwenye mabano ni usafirishaji kimataifa (6), Afrika Mashariki (2), ndani ya Tanzania (47), ndani ya miji ( 16), kati ya miji (79). Kulikuwa na leseni 148 Septemba 2024.

Kikoa cha dot tz ni utambulisho wa kipekee wa Tanzania kwenye mitandao ya intaneti, kama ilivyo msimbo wa +255 unaotambulisha Tanzania kwenye mawasiliano ya simu kimataifa.

Kuna faida lukuki za kutumia kikoa cha Tanzania. Hizi ni pamoja na wateja wa taasisi, biashara au mhusika binafsi kufikia tovuti husika kwa urahisi zaidi. Vilevile matumizi ya kikoa cha Tanzania yanaonesha weledi wa mmilki wa anwani yenye kikoa hicho na inatoa fursa kujitangaza kwa wateja wa ndani.

Kikoa cha ndani pia kinajenga imani ya wateja kwa mtoa huduma au muuzaji bidhaa mwenye anwani. Wateja wanaridhika zaidi na kuwa na aina ya kujivuna wanapotumia anwani yenye utambulisho wa kitaifa.

Wataalamu wamethibitisha kwamba watumiaji huduma na bidhaa wanajifunganisha na jina lenye ukaribu nao. Kwa mfano wengi wanakuwa na imani na kujisikia salama zaidi wanapowasiliana kwa barua pepe kupitia anwani zenye majina rasmi ya nchini kwao kuliko anwani zenye vikoa vya jumla kama vile dot com.

Vilevile ni nadra sana kwa barua pepe zenye kikoa cha nchi husika kukataliwa na mifumo mingi ya usalama wa mitandao kwenye taasisi.

Vilevile, kutumia kikoa cha ndani ya nchi kwenye tovuti au kwa mawasiliano ya barua pepe kunaipa taasisi au mhusika taswira ya weledi na kujiamini. Kunaonesha kwamba wenye tovuti au anwani ya barua pepe wamechukua juhudi za ziada kujisajili nchini mwao na kulipa ada kidogo,badala ya kutumia vikoa vya kimataifa vinavyotolewa bure.

Faida nyingine kubwa ya kutumia vikoa vya ndani ni kwenye kuwezesha taasisi au mhusika kufikiwa kwa haraka na wateja wanaotafuta bidhaa au huduma tangaza biashara. Mtu anapotafuta bidhaa au huduma mtandaoni, zikiwemo pia nyaraka au rejea mbalimbali, mitandao ya kompyuta inaanza kusaka kinachotafutwa.

Mipangilio kwenye mifumo inayosaka taarifa, kama vile 'Google' au 'Yahoo' inatambua anwani zenye maneno ambayo mtafutaji ameyaweka.



Wigo wa kusaka tovuti zenye biashara mteja aliyotaja kwa kuweka jina Tanzania ni mpana zaidi kwa tovuti za dot com.

Tovuti zenye dot tz zitakuwa juu zaidi ya nyingine. Kwa mfano, mifumo ya kusaka itam-patia mteja anayetafuta bidhaa za Tanzania tovuti zenye vikoa vya dot tz haraka zaidi kuliko vyenye dot com.

Tovuti husika kuwa juu zaidi na kupatikana kwa haraka kunaongeza imani ya watumiaji na pia kujenga taswira nzuri ya mwenye kikoa.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Dkt Jabiri Bakari amewataka Watanzania kusajili na kutumia kikoa cha Tanzania.

Taasisi za umma na kampuni za biashara zinatakiwa kisheria kusajili na kutumia vikoa vya Tanzania. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 10-(1) cha kanuni za Namba na Anwani za mawasiliano ya kielektroniki na posta.

Pamoja na kuwezesha mwenye kikoa kujitangaza, migogoro inayohusiana na vikoa inaweza kushughulikiwa kirahisi ndani ya Tanzania kuliko inayohusu vikoa vya nje.

Dkt Bakari ameeleza kuwa wenye vikoa vya dot tz wana fursa ya kuvitumia bila wasiwasi wa kufungiwa iwapo kuna matatizo tofauti na vya nje ambavyo matumizi yake yanaambatana na masharti magumu. Haya ni pamoja faini za hadi dola 100 za Kimarekani au kufungiwa kwa muda kwa ukiukwaji.

Orodha ya wasajili wenye ithibati ya shughuli hiyo kutoka TCRA imechapishwa kwenye tovuti ya https://karibu.tz/domains/registrars/.

MATUKIO

# Tanzania kuwa na kituo cha ubunifu

Na Mwandishi wetu

Tanzania inaanzisha kituo cha kitaifa cha ubunifu katika teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ili kujenga uwezo, na kuchochea ubunifu wa kidijitali nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Jabiri Bakari ameeleza kuwa kituo hicho kinalenga kuchochea mabadiliko ya ikolojia nzima ya ubunifu Tanzania.

Aidha ameongeza kuwa kituo hicho ni sehemu ya Mtandao wa vituo vya ubunifu vinavyoanzishwa na Shirika la mawasiliano ya Simu Ulimwenguni (ITU), katika ngazi za dunia,mabara/kanda na kitaifa.

Dkt Bakari, ambaye ni mjumbe wa Bodi ya Wadau wa Usimamizi wa Bunifu ya ITU, amesema kituo hicho kitatoa msaada wa kiufundi kwa vituo vya ubunifu.

Kituo hicho, kinachowezeshwa na ITU, kinasimamiwa na Tume ya TEHAMA Tanzania.



Kikao cha Bodi hiyo lilichofanyika Valetta Malta Oktoba mwaka huu kilifuatiwa na Mkutano wa kimataifa wa ubunifu, kwa kifupi GIF.

ITU ilianzisha Ushirikiano wa Ubunifu na Ujasirimali, Januari mwaka 2023 ili kuweka mfumo wa kupunguza mapengo ya ubunifu kwenye nchi wanachama.

Tanzania, kupitia TCRA, inatekeleza mpango wa kuendeleza ubunifu na uvumbuzi kwa kutoa raslimali za mawasiliano bure kwa wajasiriamali na kampuni changa kujaribu miradi yao.

Pamoja na Dkt Bakari, wawakilishi wengine wa Tanzania kwenye mkutano wa GIF Malta walikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA Dkt. Nkundwe Mwasaga, na Mkurugenzi wa Masuala ya Kisekta TCRA Mhandisi Mwesigwa Felician. Wengine ni Ezra Mmakasa wa TCRA na Dkt. Florence Rashid wa Chuo Kikuu cha Dodoma.

Dkt Bakari ameueleza mkutano huo kuwa umekuwa na tija sana. Umejadili njia za kukuza bunifu mbalimbali za TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuangalia upatikanaji wa rasilimali fedha na watu.

Vilevile wajumbe wamezungumzia njia za kukuza ushirikiano kati ya vyuo vikuu vya ubunifu na taasisi zinazojihusisha na ubunifu. Hii ni pamoja na kuwa na mfumo utakaowezesha ubadilishanaji wa taarifa za vituo vya ubunifu duniani.

Mengine ni muhimu wa kulinda haki miliki za bunifu mbalimbali na kuzikuza. Lengo ni kuwezesha wabunifu kufaidika na kazi zao.

Wajumbe pia walijadili vipaumbele kwenye ubunifu, mfano bunifu zinazolenga kusaidia upatikaji wa huduma sehemu zisizo na huduma, hasa vijijini na pembezoni.

# Sekta ya Mawasiliano katika namba

## Idadi ya laini zilizosajiliwa iliongezeka kipindi cha robo mwaka kilichoishia Desemba 2024

**80.7 milioni**
Septemba 2024

**86.8 milioni**
Disemba 2024

**7.7%** ▲

Mawasiliano ya binadamu (P2P)
**85.8 milioni** (▲7.8%)

Mawasiliano ya vifaa na mitambo (M2M)
**1.01 milioni** (▼-0.4%)


**47.2%** au **takriban nusu** ya laini za simu zilizosajiliwa nchini zinapatikana katika mikoa sita ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Dodoma na Morogoro.

**Wanaume walikuwa wana laini nyingi zilizosajiliwa kuliko wanawake katika robo mwaka iliyoishia Disemba 2024**


milioni **44.6** (51.4%)

milioni **42.2** (48.6%)

### Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma wa P2P




### Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma wa M2M





### VIFAA VINAVYOTUMIA LAINI NA KUUNGANISHWA NA INTANETI

**Simu za rununu (Feature phone)**
milioni **56.86**
Ueneaji: **87.4%**

**Simu janja (Smartphones)**
**23.41** milioni
Ueneaji: **36%**

### WATUMIAJI WA HUDUMA ZA INTANETI




**16.1%** ▲


# Akaunti za pesa mtandao zaendelea kuongezeka Tanzania

## Akaunti za pesa mtandao zimeongezeka kwa 2% katika robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2024

**60.8** milioni
Septemba 2024

**61.9** milioni
Disemba 2024

## Mgawanyo wa akaunti za pesa mtandao




# Huduma za utangazaji kwa ufupi



### Mgawanyiko wa visimbuzi vilivyolipiwa

DTH 27%

DTT 73%

### Jumla ya visimbuzi vilivyolipiwa

**2,148,763**

Dar es Salaam inaongoza kwa kuwa na visimbuzi vinavyolipiwa **703,580** sawa na **33%** ya visimbuzi vyote nchini ikifuatiwa na Mwanza yenye visimbuzi 176,792, Mbeya (148,000) na Arusha ikiwa na visimbuzi 137,534.

### Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa kwa kila mtoa huduma hadi Disemba 2024

| Mtoa huduma | DTT | DTH | Jumla |
|---|---|---|---|
| Agape Associates Limited | 1,840 | 0 | **1,840** |
| Azam Media Limited | 294,775 | 1,045,360 | **1,340,135** |
| Basic Transmissions Limited (Digitek) | 15,000 | 0 | **15,000** |
| Basic Trasnmissions Limited (Continental) | 36,413 | 31,250 | **67,663** |
| Multichoice Tanzania Limited (DStv) | 0 | 225,263 | **225,263** |
| Star Media Limited | 232,494 | 245,033 | **477,527** |
| Zuku | 0 | 21,335 | **21,335** |

# Ukuaji wazidi asilimia 20 maeneo mengi, huduma zazidi kuimarika

Na Mwandishi wetu

Maeneo mengi ya huduma za mawasiliano Tanzania yamekua kwa zaidi ya asilimia 20 kati ya Januari na Desemba 2024 na baadhi ya vidokezi vinaonesha kuongezeka mara 10 ndani ya mwaka mmoja.

Ukuaji wa zaidi ya asilimia 20 uko kwenye laini za simu, matumizi ya intaneti, Kuenea teknolojia ya mawasiliano ya mkononi  uzao wa tano (5G) na leseni za redio za jamii, vyeti vya idhini ya matumizi ya vifaa vya mawasiliano Tanzania.

Laini za simu zimeongezeka kwa asilimia 25, kutoka 70,035,043 mpaka 87,448,346; watumiaji/wasajiliwa wa intaneti  kwa asilimia 33 kutoka 36,211,559 mpaka 48,028,227 na asilimia ya watu wanaofikiwa na teknolojia ya 5G kutoka 13 hadi 50.

Simu zenye uwezo mkubwa, au simu janja zimeenea miongoni mwa watu kwa asilimia 36, kutoka asilimia 32 Januari.




Vyeti vya idhini ya matumizi ya vifaa vya mawasiliano vimeongezeka kwa asilimia 119, kutoka 2,175 mpaka 4,774. Usajili wa simu za mkononi za saeteilaiti umeongezeka mara 11, kutoka nne (4) Januari hadi 42 Desemba.

Vyeti vya mifumo ya kimataifa ya usalama na hali ya hatari majini vimeongezeka kwa asilimia 90, kutoka 103 mpaka 196.

Leseni za redio za jamii zimeongezeka kwa asilimia 55, kutoka 11 mpaka 17; za utoaji wa maudhui ya televisheni kwa malipo ngazi ya wilaya kwa asilimia 180, kutoka 10 mpaka 18.

Akaunti za pesa kwa simu za mkononi zimeongezeka kwa asilimia 16.1, kutoka 52,973,700 mpaka 61,882,499.

Vikoa vya jina la Tanzania () dot tz) vimefikia 32,267, kutoka 29,006 ikiwa ni ongezeko la asilimia 11.

Maeneo yaliyoshuka yanajumuisha yale yenye matokeo hasi na chanya. Kwa mfano matukio ya ulaghai kupitia simu za mkononi yameshuka kwa asilimia 37, kutoka 20,939 mpaka 13,120.

Leseni za kusimika mitambo ya setilaiti  imeshuka kwa asilimia 23; kutoka 47 mpaka 36. Vyeti vya kutumia namba vimepungua kwa asilimia 62, kutoka 533 hadi 200.

Pamoja na matokeo haya yanayotokana na TCRA kuendelea kusimamia sekta kwa ufanisi, Tanzania imeapaeta mafanikio mbalimbali kimataifa kwenye sekta ya mawasiliano. (Rejea makala kurasa za awali za toleo hili).

**Jedwali. Hali ya mawasiliano Tanzania mwaka 2024**

| Maelezo | Januari 2024 | Machi | Juni | Septemba | Desemba | Ongezeko | Asilimia ongezeko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Laini za simu za mkononi | | | | | | | |
| Jumla | 70,035,043 | 72,418,634 | 76,529,446 | 80,662.041 | 87,448,346 | 17,413,303 | 24.86 |
| Kuenea kwa watu | | 112 | 116 | 124 | 134% | 22 pts | |
| Laini za mtu na mtu (P2P) | 70,112,342 | 72,496,095 | 75,588,006 | 79,646,221 | 86,381,780 | 16,269,537 | 23.20 |
| Laini za mashine (M2M) | | 929,683 | 962,928 | 1,015,820 | 1,066,566 | 136,883 | 14.72 |
| 2. Huduma za intaneti | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Watumiaji/wasajiliwa | 36,211,559 | 36,771,612 | 39,311,477 | 41,376,545 | 48,028,227 | 11,816,668 | 32.63 |
| 2B. Teknolojia inayotumika kupata intaneti na idadi ya wasajiliwa/laini zilizotumika | | | | | | | |
| Simu za mkononi | 35,815,632 | 36,687,794 | 39,154,908 | 41,242,748 | 47,859,272 | 12,043,640 | 33.63 |
| 2C. Teknolojia nyingine | | | | | | | |
| Idadi ya uunganishwaji kwa nyaya za faiba hadi nyumbani (FTTH) | 61,645 | 49,163 | 50,398 | 59,743 | 83,201 | 21,556 | 34.96 |
| Idadi ya uunganishwaji kwa nyaya za faiba hadi nyumbani (FTTO) | 8,315 | 5,126 | 5,732 | 10,449 | 12,113 | 3,798 | 45.67 |
| 2D. Kasi kwenye matumizi ya intaneti (MB kwa sekunde (Megabaiti kwa sekunde - Mbps) | | | | | | | |
| Kasi ya kupakia data | | | | | | | |
| Kupitia vifaa vya mkononi | 6.14 | 11.1 | 12 | 12 | 14.9 | 8.76 | 42.67 |
| Kupitia vifaa vilivyosimikwa | 32.9 | 35.1 | 35 | 35 | 36 | 3.1 | 9.42 |
| Kasi ya Kupakua data | | | | | | | |
| Kupitia vifaa vya mkononi | 11.03 | 11.4 | 12 | 12 | 14.9 | 3.87 | 35.08 |
| Kupitia vifaa vilivyosimikwa | 34.11 | 40 | 42.1 | 40 | 42.4 | 8.29 | 24.30 |
| 3. Kuenea teknolojia ya simu za mkononi uzao wa tatu (3G), wa nne (4G), wa tano (5G) | | | | | | | |
| Asilimia ya watu wanaofikiwa na 3G | 86 | 88 | 89 | 90.1 | 91 | 5 | 5.81 |
| Asilimia ya watu wanaofikiwa na teknolojia ya 4G | 79 | 80 | 83 | 84.9 | 88 | 9 | 11.39 |
| Asilimia ya watu wanaofikiwa na teknolojia ya 5G | | 13 | 15 | 18 | 20 | 7 | 53.84 |
| Asilimia ya eneo kijiografia inalofikiwa na 3G | 70 | 72 | 73 | 73.6 | 74 | 4 | 5.79 |
| Asilimia ya eneo kijiografia inalofikiwa na 4G | 63 | 64 | 69 | 70.2 | 71 | 8 | 12.69 |
| Asilimia ya eneo kijiografia inalofikiwa na 5G | | 1 | 2 | 2.2 | 2.5 | 1.5 | 150 |

| Maelezo | Januari 2024 | Machi | Juni | Septemba | Desemba | Ongezeko | Asilimia ongezeko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. Huduma za pesa kwa simu za mkononi | | | | | | | |
| Akaunti za pesa kwa simu | 52,973,700 | 52,990,091 | 55,523,067 | 60,815,533 | 61,882,499 | 8.908.799 | 16.18 |
| 5. Ulaghai kwenye mitandao ya simu za mkononi | | | | | | | |
| Majaribio ya ulaghai kwenye mitandao ya simu za mkononi | 20,939 | 17,318 | 22,257 | 16,002 | 12,896 | 7,819 | 37.34 |
| 6. Utangazaji | | | | | | | |
| Ving'amuzi vya televisheni mfumo wa mitambo ya ardhini (DTT) na saeteilaiti (DTH) | 3,661,976 | 3,752,170 | 3,843,694 | 2,175,810 | 2,148,763 | 1,513,213 | 41.32 |
| Ving'amuzi vya waya | 16,223 | 15,781 | 18,820 | 19,153 | 16,767 | 544 | 3.35 |
| Asilimia ya watu wanaofikiwa na mawimbi ya televisheni mfumo wa mitambo ya ardhini (DTT) | 56 | 56 | 58 | 58 | 2 pts | 2.83 | |
| Asilimia ya watu wanaofikiwa na mawimbi ya televisheni mfumo wa mitambo ya saeteilaiti (DTH) | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | | |
| Asilimia ya watu wanaofikiwa na mawimbi ya utangazaji ya FM | | | 75.85 | 75.52 | 78 | 78 | 2.15 |
| Asilimia ya eneo la kijiografia linalofikiwa na televisheni mfumo wa mitambo ya ardhini (DTT) | | | 32 | 32 | 33 | 33 | 1 |
| Asilimia ya eneo la kijiografia linalofikiwa na mfumo wa mitambo ya televisheni kupitiasetilaiti (DTH) | | 100 | 100 | 100 | 100 | | |
| Asilimia ya eneo la kijiografia linalofikiwa na mawimbi ya utangazaji ya FM | 55.14 | 49.9 | 56.5 | 56.5 | 1.36 | | |
| 7. Huduma za Posta na usafirishaji vifurushi | | | | | | | |
| Kwa kutumia vidokezi vya huduma za posta na usafirishaji vifurushi zimeonesha mwelekeo wa kupanda na kushuka kwenye maeneo mengi. Aidha, takwimu nyingi zinatokana na huduma zinazotolewa na Posta ya umma - Shirika la Posta Tanzania. | | | | | | | |
| Nyaraka | 138,981 | 139,419 | 223,997 | 169,415 | 146,004 | 7023 | 5.5 |
| Barua | 469,055 | 1,101,230 | 155,831 | 166,590 | 168,983 | 299,072 | |
| 7B. Vitu vilivyopostiwa kwenda nchi za Afrika Mashariki na penginepo duniani | | | | | | | |
| Nyaraka | 12,290 | 13,420 | 9,456 | 8,690 | 9,075 | 3,215 | |
| Barua | 143,145 | 84,477 | 33,934 | 15,078 | 43,998 | 99,147 | |
| 8. Kuenea kwa vifaa vilivyounganishwa kwenye mitandao ya mawasiliano | | | | | | | |
| Simu za kawaida/simu rununu | 85.62% | 85.56% | 82.60% | 84.83% | 87.39% | 1.77% | 41.32% |
| Simu janja | 33.13% | 32.59% | 31.55% | 33.85% | 35.99% | 3.86% | |
| Vifaa vya kushika mkononi | 2.75% | 2.68% | 2.49% | 2.44% | 2.50% | 0.25% | |

| Maelezo | Januari 2024 | Machi | Juni | Septemba | Desemba | Ongezeko | Asilimia ongezeko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Modemu | 0.95% | 0.98% | 0.97% | 1.00% | 1.02% | 0.07% | |
| Vishkwambi | 0.65% | 0.67% | 0.68% | 0.67% | 0.74% | 0.09% | |
| Router za WLAN | 0.18% | 0.21% | 0.22% | 0.27% | 0.32% | 0.14% | |
| Dongle | 0.16% | 0.17% | 0.15% | 0.15% | 0.15% | 0.01% | |
| Vifaa vinavyoweza kuwasiliana vyenyewe kupitia intaneti | 0.15% | 0.19% | 0.19% | 0.21% | 0.32% | 0.17% | |
| 9. Vikoa vya jina la Tanzania (dot tz) | | | | | | | |
| Vikoa vilivyosajiliwa | 29,006 | 29,968 | 30,698 | 31,584 | 32,267 | 3,261 | 11.24 |
| 10A. Leseni limbikizi zilizotolewa hadi Desemba ( mawasiliano ya simu) | | | | | | | |
| Miundombinu ya mawasiliano | 36 | 35 | 34 | 35 | 37 | 1 | 2.71 |
| Huduma za mtandao wa mawasiliano | 17 | 14 | 15 | 16 | 18 | 1 | 5.88 |
| Huduma za mfumo na programu tumizi | 146 | 135 | 142 | 146 | 155 | 9 | 6.15 |
| Huduma za usalama mtandaoni | | | | 33 | 37 | 4 | 12.12 |
| Huduma za mfumo na programu tumizi – biashara mtandao | Leseni hii ilianzishwa 2024 kufuatia marekebisho ya Kanuni za leseni. Tanzania inaimarisha miundombinu wezeshi na mifumo muhimu ya kuendeleza biashara mtandao. | | | 5 | 5 | | |
| Aircraft Stations | 163 | 171 | 169 | 176 | 178 | 15 | 9.20 |
| Mitambo iliyosimikwa ya madishi ya satilaiti | 47 | 45 | 42 | 36 | 36 | 11 | 23.40 |
| Mitambo inayohamishika ya madishi ya satilaiti | 2 | 2b | 2 | 2 | 2 | | |
| Stesheni za ardhini za satelaiti | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | | |
| Ship Stations | 45 | 47 | 35 | 36 | 30 | 5 | 33.33 |
| Mitambo ya redio za mawasiliano, zikiwa ni pamoja na zinazotumia masafa ya za HF, VHF, UHF na vituo unganishi vya VHF na UHF. Humu pia zimo leseni za mitambo ya VHF na UF ya masafa aina moja au jozi (HF Radio Stations, VHF- UHF Radio Repeaters, VHF - UHF Radio Station with Pair of Frequency, VHF - UHF Radio Station with Single Frequency). | | | | | | | |
| Mitambo ya redio za mawasiliano | 348 | 342 | 335 | 316 | 318 | 30 | -8.6 |
| Namba na misimbo | 533 | 536 | 576 | 493 | 200 | 333 | 62.47 |
| Mifumo ya kimataifa ya usalama na hali ya hatari majini | 103 | 132 | 152 | 177 | 196 | 93 | 90.26 |
| Idhini ya vifaa vinavyotumika Tanzania | 2,175 | 2,281 | 2,426 | 4,590 | 4,774 | 2,596 | 119.49 |
| Usajili wa simu za mkononi za satilaiti | 4 | 12 | 32 | 32 | 46 | 42 | (1050)x11 |
| 10B. Leseni limbikizi zilizotolewa hadi Desemba (utangazaji wa televisheni zisizolipiwa – FTA) | | | | | | | |
| FTA Taifa | 17 | 16 | 16 | 16 | 17 | 0 | |

| Maelezo | Januari 2024 | Machi | Juni | Septemba | Desemba | Ongezeko | Asilimia ongezeko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| FTA ngazi ya wilaya | 20 | 24 | 23 | 22 | 21 | 1 | 5 |
| Redio taifa | 13 | 14 | 14 | 14 | 14 | 1 | 7.69 |
| | | | | | | | |
| Redio mkoa | 32 | 31 | 31 | 33 | 33 | 11 | 3.1 |
| Redio wilaya | 165 | 169 | 177 | 182 | 186 | 21 | 12.72 |
| Redio za jamii | 11 | 17 | 15 | 17 | 11 | 6 | 54.54 |
| Televisheni za kulipia kitaifa | 10 | 16 | 25 | 28 | 28 | 18 | 180 |
| Televisheni za kulipia wilaya | 2 | 9 | 1 | 1 | 1 | 1 | 50 |
| Televisheni kwa waya | 56 | 60 | 63 | 63 | 58 | 2 | 11.53 |
| Watoa huduma za kiufundi za utangazaji | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | | |
| 10C. Leseni limbikizi zilizotolewa hadi Desemba (huduma za maudhui mtandaoni) | | | | | | | |
| Waandaji na wapangaji wa maudhui mtandaoni | 3 | 3 | 5 | 6 | 6 | 3 | |
| Blogu | 60 | 67 | 64 | 66 | 66 | 6 | 10 |
| Redio mtandaoni | 6 | 7 | 9 | 10 | 10 | 4 | 66.66 |
| Televisheni mtandaoni | 220 | 231 | 215 | 210 | 199 | 21 | 9.54 |
| 10D. Leseni limbikizi zilizotolewa hadi Desemba (Posta na Usafirishaji Vifurushi) | | | | | | | |
| Usafirishaji kimataifa | 6 | 6 | 8 | 6 | 6 | | |
| Usafirishaji Afrika Mashariki | 1 | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 100 |
| Usafirishaji kati ya miji | 50 | 65 | 71 | 76 | 79 | 29 | 58 |
| Usafirishaji ndani ya miji | 14 | 15 | 18 | 16 | 18 | 4 | 28.87 |
| Mtoa huduma za Posta wa Umma | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | | |
| Usafirishaji ndani ya nchi | 45 | 46 | 46 | 47 | | 2 | 4.44 |

Mawasiliano Towers,
20 Sam Nujoma Road,
14414 Dar es Salaam, Tanzania.
Email: dg@tcra.go.tz

@tcra_tanzania